JIBU: Kama ulishawahi kuwahubiria watu kadha wa kadha habari za wokovu, naamini ulishawahi kukutana na watu baadhi wakikueleza, maneno haya, kwamba haijalishi wewe ni dini gani, au unaamini nini, imani yako ndiyo itakayokuokoa, ukiwa na imani kuwa Mungu yupo, hilo tu, linakutosha, hayo mengine si ya muhimu sana.

Atakuambia hata anayeabudu kupitia mti, au anayeabudu kupitia ng’ombe Mungu anamsikia hata, anayeabudu kupitia Rozari Mungu anamsikia kinachojalisha ni imani yake tu wala si kingine.

Ni kweli kabisa mawazo yao ni sahihi, kwamba imani ni daraja la kumfikia Mungu, kama vile maandiko yanavyosema katika..

> *Waebrania 11:6 “Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao”.*

Lakini hawajui kuwa Imani ambayo haijakamilishwa haikufikishi popote, nikiwa na maana imani ambayo haijulikana msingi wake

ni upi, imejengwa katika nini haikupeleki popote.. Kitendo cha kuamini tu Mungu yupo, hata wachawi wanaamini hivyo, na ukiwauliza watakuambia ndio namwamini Mungu na pia ananisaidia, mapepo nayo yatakuambia sisi nasi tunamwamini Mungu na pia tunatetemeka tunapolisikia jina lake..

Utalithibitisha hilo katika..

> *Yakobo 2:19 “Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja; watenda vema. Mashetani nao waamini na kutetemeka”.*

Sasa kama unasema mimi naamini Mungu, na namwogopa, ujue kuwa huna tofauti na mashetani. Kama unadhani utakwenda mbinguni kwa imani ya namna hiyo, basi ujue mashetani watakutangulia kwanza mbinguni kisha wewe utayafuata baadaye.

Bwana Yesu alisema wazi kabisa katika Yohana 14:6..”mimi ndio njia na kweli na uzima, mtu hafiki kwa Baba isipokuwa kwa njia yangu mimi.” Akiwa na maana hakuna imani yoyote itayokufikisha mbinguni isipokuwa ile ya kumwamini yeye (Yesu

Kristo).

Ni sawa na leo useme unayo simu, yenye line nzuri, yenye salio la kutosha, hivyo unaweza sasa kuwasiliana na mimi wakati wowote.. Jibu ni la! kama hutakuwa na namba yangu ya simu, kamwe hutakaa uwasiliane na mimi.. Haijalishi utakuwa na simu nzuri, au salio la kutosha au namba za watu wengine elfu kwenye kitabu chako cha kumbukumbu, kama huna namba yangu mimi binafsi, kamwe huwezi kuwasiliana na mimi.

Leo hii watu wanataka kuwasiliana na Mungu, kwa njia zao wenyewe walizojitungia, wanajaribu kupiga kila namba wanayoibuni tu vichwani mwao, wengine wanamtafuta Mungu kupitia dini zao, wengine wadhehebu yao, wengine wanyama, wengine miti,sanamu, jua, mwezi, n.k. wakidai kuwa wanamtafuta Mungu Yule Yule mmoja, ukiwaeleza dini au dhehebu halikufikishi popote, watakuambia usitupotoshe, imani yako ndio itakayokuokoa..

Ndugu, usipomuamini Yesu, hutafika popote. Na kumwamini Yesu sio kusema mimi ni mkristo, au mimi namwamini Yesu, hapana, bali kunakuja kwa kutubu kwanza dhambi zako kwa kumaanisha kuziacha, pili kwa kubatizwa katika ubatizo sahihi wa kuzamishwa

katika maji tele katika jina lake sawasawa na Matendo 2:38, Kisha kupokea Roho Mtakatifu. Na kuanzia hapo kuishi maisha matakatifu yanayoendana na Neno lake,(yaani BIBLIA). Sasa Kwa kufanya hivyo imani yako itakuwa imekamilishwa mahali sahihi. Hapo ndipo utakuwa na uhakika unamwabudu Mungu kweli, kupitia mwana wake Yesu Kristo.

Lakini kwa kusema tu mimi namwamini Mungu, imani yangu itaniokoa na huku hujui Mungu kakuagiza nini katika Neno lake, au anakutaka ufanye nini..Ujue kuwa umepotea, na ukifa leo utakwenda kuzimu. Vilevile ukijivunua dhehebu lako, na hutaki kumtafuta Kristo Yesu aliye njia, ujue kuwa kuzimu itakuwa pia ni sehemu yako. Hakuna njia za kubuni buni katika kumfikia Mungu.. Ni sharti umwamini Yesu, na kuoshwa dhambi zako na yeye.

Maran Atha.

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema,

Kwa maombezi/Ratiba za ibada/ Ushauri/ Maswali.
Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

pia kama utapenda uyapate mafundisho haya kwa njia ya

Whatsapp au email basi tutumie ujumbe kwenye namba hizo hizo.

Mada Nyinginezo:

> *CHANGIA SASA.*

> *KITABU CHA YUDA: SEHEMU YA 1*

> *NITAUPATAJE UPENDO WA KI-MUNGU NDANI YANGU?*

> *Nini maana ya “kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi?”*

CHUKIZO LA UHARIBIFU

Rudi nyumbani

Share on:
WhatsApp